

# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

MKOA WA DODOMA



Tel.: 2354817/2321550  
Fax: 2321550

Tarehe: 14 Juni, 2019

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwataarifu watumishi na wananchi kwa ujumla kuwa kuanzia tarehe 16-23 Juni, 2019 ni wiki ya Utumishi wa Umma. Wiki hiyo itaongozwa na kaulimbiu isemayo **"Uhusiano kati ya uwezeshaji wa vijana na usimamizi wa masuala ya uhamiaji: Kujenga utamaduni wa Utawala Bora, matumizi ya TEHAMA na ubunifu katika utoaji wa Huduma Jumuishi."**

Katika Maadhimihi hayo, Halmashauri ya Jiji la Dodoma itatumia wiki hiyo mahususi kusikiliza maoni na changamoto wanazokutana nazo watumishi katika kutekeleza majukumu yao na wadau wa nje kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa na Halmashauri.

Katika wiki hiyo, Halmashauri pia itafanya usafi katika maeneo ya wananchi wanapopata huduma ya Hospitali, Masoko, Stendi na kusikiliza maoni ya wananchi na kisha kufanya ufanuzi wa hoja zitakazotolewa.

Halmashauri ya Jiji imetenga chumba cha ofisi (namba 72) maalum kwa ajili ya kusikiliza malalamiko, maoni, hoja na ushauri kutoka watumishi na wananchi kwa ujumla kuanzia saa 2:00 asubuhi nadi saa 9:30 alasiri. Pia watumishi na wananchi wanashauriwa kutumia Mabox ya maoni yaliyopo katika ofisi za Halmashauri.

Taarifa hii imetolewa na:-

Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano

Halmashauri ya Jiji

DODOMA